**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA.**

**WIZARA YA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM.**

**Chuo cha Maendeleo ya Jamii -Ruaha**

S.L.P 254
**IRINGA**
16/05/2022

Simu:255262725152
Barua Pepe :pruaha@jamii.go.tz
Fax: 25526275152
Tovuti: www.ruahacdti.ac.tz

TAREHE.........................................................................

Ndugu............................................................................

## YAH: KUCHAGULIWA KUJIUNGA NA MAFUNZO YA CHETI CHA AWALI (NTA LEVEL 4) CHA MAENDELEO YA JAMII KATIKA CHUO CHA MAENDELEO YA JAMII RUAHA, MWAKA WA MASOMO 2022/2023.

**1:0** Hongera!! Umechaguliwa kujiunga katika mafunzo ya Taaluma ya Maendeleo ya Jamii ngazi ya Cheti **(NTA LEVEL 4).** Mafunzo haya ya mwaka mmoja yatakuwezesha kupata Cheti katika fani hiyo. Utatakiwa kushiriki kikamilifu katika mafunzo ya nadharia darasani na mafunzo kwa vitendo.

**2:0** Mafunzo hayo yanaendeshwa katika Chuo cha Maendeleo ya Jamii Ruaha kilichopo katika Manispaa ya Iringa barabara kuu iendayo makao makuu ya Wilaya ya Kilolo.

**3:0** Chuo kitafunguliwa **tarehe 10/10/2022** na unatakiwa uwe umefika chuoni si zaidi ya **tarehe 24/10/2022**.Iwapo hutofika baada ya tarehe hiyo nafasi yako itachukuliwa na mtu mwingine.Masomo yataanza rasmi tarehe **18/10/2022**

**4:0** Taratibu za malipo ya ada na michango mingine ya chuo ni kama ifuatavyo:

**4:1** Mwanachuo anatakiwa kulipa fedha za kugharamia mafunzo ya chuo yaani ada shilingi laki sita tu (**600,000/=**) (fedha hii inaweza kulipwa kwa awamu mbili) utaratibu wa kulipa wasiliana na chuo kwa ajili ya kutengenezewa namba ya malipo ya serikali.

**4:2** Mchango wa bweni ni shilingi laki mbili **(200,000/=)** kwa mwaka, kwa muhula wa kwanza unatakiwa kulipa shilingi laki moja **(100,000/=)** na muhula wa pili shilingi laki moja **(100,000/=)** Utaratibu wa kulipa wasiliana na chuo kwa ajili ya kutengenezewa namba ya malipo ya serikali.

**4:3** Michango mingine ya chuo ni shilingi laki moja na elfu hamsini na tano na mia nne tu.( **155,400/=)** (ilipwe yote kwa mara moja) utaratibu wa kulipa wasiliana na chuo kwa ajili ya kutengenezewa namba ya malipo ya serikali. (control number)

**4:4** Pia mwanachuo anatakiwa kulipa shilingi elfu kumi tu (**10,000/=)** kwa ajili ya mchango wa serikali ya wanachuo kwenye akaunti namba **60510007149-NMB – MKWAWA BRANCH IRINGA. JINA LA AKAUNTI RUAHA STUDENT'S ORGANIZATION.**

**4:5** Wakati wa mafunzo kwa vitendo yaani (field attachment)ambayo yatafanyika mwanzoni mwa muhula wa pili,mzazi atapaswa kumgharamia mwanafunzi fedha ya kujikimu katika kipindi hicho kulingana na eneo atakapofanyia (fedha hiyo imekadiriwa kuwa shilingi **300,000/=)** fedha hiyo hailipwi chuoni ni ya mwanafunzi kwa hiyo apewe mwanafunzi mwenyewe.

JEDWALI :1 Mchanganuo wa malipo ya ada na michango mingine ya chuo ni kama ifutavyo;

| **MAELEZO** | **KIASI KWA MWAKA** | **NUSU** | **AKAUNTI** |
|---|---|---|---|
| **Ada** | **600,000/=** | **300,000/=** | **CONTROL NUMBER** |
| **BWENI** | **200,000/=** | **100,000/=** | **CONTROL NUMBER** |
| **MICHANGO MINGINE** | **155,400/=** | **ILIPWE YOTE** | **CONTROL NUMBER** |
| **SERIKALI YA WANACHUO** | **10,000/=** | **ILIPWE YOTE** | **60510007149-NMB** |

**NB:Mzazi/Mlezi anaweza kutumia mchanganuo ufuatao katika ulipaji wa Ada na michango yote ya Chuo kama hatoweza kutumia jedwali namba moja.**

## MCHANGANUO WA ULIPAJI WA ADA NA MICHANGO YA CHUO

Jedwali :2

| **NTA LEVEL 4** | **ADA YA MUHULA WA KWANZA** | **AWAMU YA KWANZA 17/10/2022** | **AWAMU YA PILI 17/12/2022** | **AWAMU YA TATU 17/01/2023** |
|---|---|---|---|---|
| BWENI | 505,000/= | 170,000/= | 170,000/= | 165,000/= |
| KUTWA | 405,000/= | 135,000/= | 135,000/= | 135,000/= |

- **Hakikisha malipo yote yafanyike kwa utaratibu wa kutengenezewa namba ya malipo ya serikali (control number).**
- **Kwa kuwasiliana na Mhasibu wa Chuo kwa namba 0752-181915/0718-811124/0625-927058**
- **Bima ya afya ni lazima kwa kila mwanachuo.**

Michango mingine ni gharama ya afya 50,400/= Tear and wear (fedha ya uchakavu hairudishwi) 10,000/=,usajili wa mwanachuo 15,000/= kitambulisho 10,000/= first Aid 10,000/= certificate and transcript 15,000/=examination fee 30,000/=na gharama ya usajili wa NACTE 15,000/=jumla ya michango yote hii ni shilingi 155,400/=

**5:0** Gharama za usafiri wa kwenda chuoni na kurudi nyumbani kwa mihula yote itakuwa ni jukumu la mzazi/mlezi.

**6:0** Mara utakapofika chuoni utatakiwa uwasilishe;

- ✓ Cheti halisi (original) cha kidato cha nne ( pamoja na kivuli chake) au taarifa ya matokeo ya mtihani (statement of result) kwa wale waliomaliza kidato cha nne mwaka 2021 tu,pamoja na kivuli chake.
- ✓ Cheti cha kuzaliwa(orginal) pamoja na kivuli chake yani copy.
- ✓ Picha tatu(3) passport size zilizo pigwa hivi karibuni.

- ✓ Blanketi 1, shuka 2, mto,ndoo,vyombo vya kulia chakula,nguo za michezo (track suit) na chandarua cha mbu kwa matumizi yako mwenyewe.

**7:0** Mara ufikapo chuoni utapewa kanuni na taratibu za chuo pia utapata fursa ya kujizoeza na mazingira ya chuo (orientation).

**8:0** Mavazi ya heshima kwa wanachuo wote ni muhimu,suruali kwa watoto wa kike haziruhusiwi.

**8:1** Vitu hatarishi (kama kisu,bangi,misumeno na nondo haviruhusiwi maeneo ya chuo

**9:0** Iwapo unakubaliana na masharti uliopewa hapo juu,tafadhali jaza na weka saini yako pamoja na mzazi /mlezi katika fomu iliyoambatanishwa na kabidhi ofisi ya usajili (admission office).

**10:0** Mwanafunzi atajigaramia chakula akiwa chuoni ambayo ni shilingi 850,000/= kwa mwaka, Muhula wa kwanza 425,000/= na Muhula wa pili 425,000/= huduma hiyo inapatikana kwa wazabuni walioteuliwa na chuo kutoa huduma ya chakula.

**11:0** Kwa mara nyingine tena nakupongeza kwa kuchaguliwa kwako kujiunga na chuo kwa ngazi ya cheti cha awali cha maendeleo ya jamii, endapo utahitaji ufafanuzi zaidi,tafadhali wasiliana na chuo S.L.P 254,Iringa au simu namba **0717-767549** .Ofisi ya usajili au NAMBA YA MKUU WA CHUO **0787080646.**

Godfrey M. Mafungu

**Mkuu wa Chuo**

PRINCIPAL
RUAHA COMMUNITY DEV. TRAINING INSTITUTE
P.O. Box 254
IRINGA

**KUBALI KUTEKELEZA MASHARTI YA KUJIUNGA NA MAFUNZO YA CHETI CHA AWALI CHA MAENDELEO YA JAMII MWAKA WA MASOMO 2022/2023**

Mimi........................................................................................................................................

**(jina kwa herufi kubwa)**

Nimepokea taarifa ya kuchaguliwa kujiunga na mafunzo ya cheti cha awali cha maendeleo ya jamii yanayotolewa katika chuo cha Maendeleo yaJamii Ruaha – Iringa

Kwa hati hii nathibitisha kwamba nitatekeleza masharti yote niliyopewa katika barua ya kuchaguliwa kwangu kujiunga na mafunzo hayo pamoja na kanuni nilizopewa na chuo.

.................................................. ..................................................

Sahihi ya mwanafunzi sahihi ya shahidi(mzazi /mlezi)

................................................ ..................................................

Tarehe sahihi ya shahidi

**FORM FOR MEDICAL EXAMINATION**

**RUAHA COMMUNITY DEVELOPMENT TRAINING INSTITUTE**

**P.O BOX 254**

**IRINGA – TANZANIA**

**TO BE COMPLETED BY Medical Officer in respect of all entrant (Applicant)**

1. Full name ..........................................................................................
2. Age .................................... Year ................................ Sex ......................
3. Blood Count (Red and White) ............................................................
4. Stool examination ................................................................................
5. Urine analysis .......................................................................................
6. Syphilis test ...........................................................................................
7. Eye test .................................................................................................
8. TB test ...................................................................................................
9. Ears .......................................................................................................
10. Chest ...................................................................................................
11. Spleen ..................................................................................................
12. Abdomen .............................................................................................

**ADDITIONAL INFORMATION: Eg. Physical Disability (If any)**

.......................................................................................................................

.......................................................................................................................

.......................................................................................................................

I certify that the above named student is fit to pursue studies

Signature ................................................ Designation ........................................
Section .................................................. Date ........................................................
Official stamp ..................................................

**STUDENT**

You must bring this complete when you come to College. No student may be enrolled without certificate of physical fitness.